# UFUNDISHAJI WA FASIHI SIMULIZI KATIKA SEKONDARI

M.L.Balisidya (Matteru)

Ufundishaji wa Fasihi Simulizi kama somo una umri mfupi katika Shule zetu za Sekondari; ingawa kwa hakika somo hili limekuwa likifunzwa hapa na pale bila ya makubaliano rasmi. Kwa mfano methali, nahau, na vitendawili vilipofunzwa darasani katika somo la Kiswahili; na vile vile nyimbo mbalimbali zilipotumiwa katika vikundi vya ngoma vya shule hapa na pale. Kutokana na hali hii tatizo lililopo leo hii, wakati tumeamua kufundisha fasihi simulizi darasani ni tuifundisheje.

Kujua namna ya kuifundisha fasihi simulizi kunategemea sana kuifahamu dhana yenyewe ya fasihi simulizi na taaluma yake. Ingawa yapo maandishi mengi katika lugha za kigeni yanayoieleza dhana hii ya fasihi simulizi, yapo maandishi machache tu ya aina hiyo kwa lugha ya Kiswahili.[1] Kwa hiyo, ili kuifahamu fasihi simulizi kinadharia semina mbalimbali zimekuwa zikiendeshwa kufuatia uelekeo huo. Kutokana na semina hizo vijiandiko na makala mbalimbali yametolewa[2] kusaidia kukuza taaluma hiyo kwa lugha ya Kiswahili. Hali hii itamsaidia mwanafunzi na mwalimu wa fasihi simulizi kujikimu kitaaluma maadam ni vigumu kuyafikia maandiko mengi yaliyo katika lugha za kigeni, kwa vile lugha hizo ama hatuzijui na kama tunazijua vitabu vyake ni aghali sana kuvipata hapa nchini kwa wingi.

Hata hivyo, pamoja na kwamba taaluma ya fasihi simulizi imeanza kushughulikiwa kinadharia kwa Kiswahili, tatizo la namna ya kukabili mada za taaluma hii katika madarasa na vidato vya shule zetu bado lingalipo na lipo kwa uzito mkubwa. Iwapo tatizo hili halitatatuliwa, somo hili halitafunzwa vizuri na huenda athari za jambo hili zitakazojitokeza hapo baadaye ni zifuatazo:

(a) Kupoteza uzito wa somo lenyewe.

(b) Kulifanya somo lishindwe kuleta na kuonyesha mabadiliko ya kielimu tunayoyategemea kutoka kwa watoto wetu hatimaye.

Kutokana na tatizo tuliloliona, basi, ina maana kwamba juhudi zo zote za kutafuta mbinu za kufundishia sasa hivi ni za awali na zipo katika majaribio tu. Ni juu yetu wote kufanya kazi kwa pamoja ili tufikie mahali pa kupata njia zilizo bora za kukabili somo hili. Yatakayotokana na makala haya, ni mapendekezo tu na kwa kujaribisha tunaweza kupata pahali pa kuanzia katika jukumu letu la kufundisha.

Kwa vile tunazingatia zaidi shule zetu za Sekondari ni vizuri kutaja kuwa mazingira ya somo hili na ufundishaji wake yatakuwa ni hapa hapa Tanzania.[3] Mifano na maelezo kuhusu sehemu nje ya Tanzania ni ya kusaidia kuliimarisha somo tu, na si ya lazima sana. Mifano hiyo itumiwe kwa nadra, inapoyumkinika.

Kwa kutaja jambo hili tunakabili pia tatizo jingine nalo ni la kushughulikia fasihi simulizi ya Tanzania. Je fasihi ya aina hiyo? Itabidi tujiulize, ni vigezo gani tutavitumia kuamua kuwa hii ndiyo fasihi simulizi ya Tanzania: Lugha? Utamaduni mzima? Siasa? Ili fasihi simulizi hiyo tunayofunza katika shule zetu ikidhi matakwa ya lengo la kufunzia somo hili, shuleni, inabidi iweze kuuwakilisha huo Utanzania ndani yake. Kwa hivi sasa fasihi simulizi hiyo tunayoifuatilia inatokana na makabila zaidi ya 130 yaliyoko Tanzania.

Fasihi Simulizi hufunzwa katika somo la lugha ya Kiswahili, hii ni lugha ya Taifa. Na tungo za Fasihi Simulizi zinazotumiwa darasani zimo katika lugha 130 ndogo ndogo. Kutokana na hali hii ukinzano baina ya Utanzania na ukabila katika somo hili la fasihi simulizi inabidi usuluhishwe. Tutafunza fasihi simulizi ya kikabila: ya Kigogo, Kizaramo, Kikuria, Kingoni? au ya Kiswahili? Je Fasihi Simulizi ya Kiswahili ipo? ni ipi?

Kabla ya kujua Fasihi simulizi ya Kiswahili ni ipi lazima tuone, je Waswahili, hao waundao fasihi ya Kiswahili ndio nani? Kuna mitazamo miwili. Labda tuiite (a) ya kale na kimapokeo na (b) ya usasa (na yenye upana zaidi). Waswahili, kimapokeo ni wale watu wa pwani ya Afrika ya Mashariki ambao wameibukia katika kukisema Kiswahili na wanamaliza maisha yao katika matumizi ya lugha hiyo. Watu hawa hawana lugha yo yote nyingine isipokuwa Kiswahili. Watu hao ni kama vile Waunguja, Wapemba, Wamvita, Waamu, Wapate na kadha kama hao. Pia baada ya misafara ya Waarabu na kuenea kwa dini hali hiyo ilijichomeza bara. Huko kukawa kuna watu ambao wanazaliwa katika Kiswahili na kulelewa na lugha hiyo, basi, hawana lugha nyingine waijuayo. Lakini leo hii kwa kuwa Kiswahili kimeenea sana katika sehemu kubwa ya bara ya Tanzania na jirani (kimeenea kwa nyenzo kadha kama vile mahubiri ya dini, utetezi na mkikimkiki wa siasa, elimu na utawala na kuenea kwa vyombo vya habari na magazeti). Basi, Kiswahili kimekiuka ile mipaka ya kuwa kina wenyewe. Kwa hivyo, kila atumiaye Kiswahili sasa kama ni lugha yake ya matumizi katika kazi, mazungumzo, arusi, jando na kadha wa kadha, huyo ni Mswahili. Dhana finyu ya watu waitwao Waswahili sasa imepanuka.

Shihabuddin Chiraghdin, "... Kiswahili kimekuwa lugha ya taifa si kwa kuwa ni lugha isiyokuwa na wenyewe bali ni lugha ambayo kila mtu wa kila kabila na rika katika taifa zima adai kuwa ni yake"[5].

Aidha upo ushahidi wa kihistoria unaotolewa na wataalamu kadha, akiwemo Guthrie na Greenberg[4] unaodhihirisha kuwa Kiswahili kinatokana na kikoa cha lugha za Kibantu. Kwa hali hiyo amali kadha za utamaduni zilizomo katika sanaa ya lugha, (fasihi simulizi) zinafanana katika makabila mengi ya Kibantu. Si ajabu kuona mithali, vitendawili, hadithi, nyimbo na fani nyingine za fasihi hiyo zinafanana au zina uhusiano mkubwa; kimaudhui, hata kimvundo. Kwa mawazo haya, basi, fasihi simulizi ya Kiswahili ipo, sio Uswahilini tu, bali pia katika makabila mengine ya Kibantu, tofauti ni lugha ya masimulizi.

Kwa ajili ya maelezo hayo twaona kuwa Fasihi Simulizi ya Kiswahili ipo. Lakini kwa kuwa Kiswahili bado kinakua kinabwia na kukumbatia tamaduni za makabila mbalimbali ya watu wenye mazingira ya Kiswahili yatubidi tuweke wazi aina za fasihi simulizi ya Kiswahili.

(a) - Ni zile nyimbo, mashairi, vitendawili, mithali na tanzu nyingine zilizoibukia katika vinywa vya Waswahili wenyewe. Zinasimuliwa na kupokewa au kutumbuizwa kwa lugha ya Kiswahili kiasili.

(b) - Ni zile nyimbo, mashairi, vitendawili na mithali pamoja na tanzu nyingine ambazo kwa asili hazitokani na wazungumzaji wa Kiswahili. Lakini kwa ajili ya uhusiano wa lugha hii na lugha za msingi mmoja; aidha, mahitaji ya lugha na mila za utaifa; tanzu mbalimbali za kikabila zinapotafsiriwa au kutumiwa kwa Kiswahili zitakubalika kuwa ni sehemu ya fasihi simulizi ya Kiswahili. Mfano mzuri ni wimbo maarufu wa TANU yajenga nchi. Madhali Kiswahiki kinakua na kuenea kupita na kukumba utajiri wa amali za makabila mbalimbali ya Tanzania na Afrika Mashariki, amali zote hizo tutazikubali kuwa mali ya fasihi simulizi ya Kiswahili. Yaani fasihi simulizi ya taifa ambalo lugha yake ya mawasiliano ni Kiswahili.

Kwa hiyo katika shule zetu za Sekondari walimu watafunza fasihi simulizi ya Tanzania kwa kutumia lugha ya Kiswahili kutokana na mifano anuai ya fasihi hiyo kama ilivyo katika makabila mbalimbali ya Tanzania.

Kurundisha Fasihi Simulizi.

Ili kufundisha somo lo lote yapo malengo maalumu ya jumla na yale mahususi. Malengo ya ufundishaji wa fasihi simulizi yameelezwa katika Kiongozi cha Mwalimu 1978. Kwa jumla ya maneno ni kwamba baada ya mwanafunzi kuhitimu katika kidato cha nne, ufundishaji wetu unatakiwa uwe umemwezesha kuwa na nadharia madhubuti za kumfanya aitambue dhana ya fasihi simulizi na kanuni mbalimbali za mwenendo wake; na dhima na dhamana yake katika jamii, ili aitumilie katika kuelewa, kufahamu na kuweza kuifanya itumike kukabili masuala mbalimbali yatokanayo na mfumo wa maisha aliyomo. Pili kijana huyo aweze kuwa ni sehemu ya uumbaji, utumizi na uenezaji wa fasihi hiyo kwa njia yo yote iliyo katika uwezo wake: njia za kimaendeleo: redio, televisheni, au vinginevyo.

Kutokana na malengo na madhumuni hayo ya jumla mwalimu atachota mada za kufundishia somo lake akitegemea uwezo na kiwango cha wanafunzi wake. Makusudi ya kufunza yatategemea msingi huo. Kwa mfano kwa kuzingatia uwezo na kiwango cha wanafunzi wa kidato cha kwanza vipengele maalumu vimetengwa, tazama Kiongozi cha mwalimu (1978) uk. 4-6. Lakini, ili kufunza vipengele hivyo kwa ukamilifu, mada zitachaguliwa na mwalimu kukidhi mahitaji maalum ya vipengele hivyo. Vipengele vinne vimeteuliwa kwa kidato cha kwanza:

1. Fasihi ni nini?
2. Fasihi Simulizi ni nini?
3. Tanzu za Fasihi Simulizi ni zipi?
4. Dhamana za Fasihi simulizi ni zipi?

Vipengele hivi vitafunzwaje. Vipindi vingi vitatakiwa kufunza kila kipengele kimoja. Kwa mfano yawezekana sana vipindi (vya dakika 40) vitatu vikatumiwa kufunza kipengele cha kwanza peke yake (na hata hivyo ni kwa kujibana tu). Kwa hiyo mwalimu atapaswa kukigawa kipengele hicho katika sehemu tatu. Mathalani:

1. Fasihi ni nini?
   (a) Ni sanaa
   (b) Ni sanaa ya maneno
   (c) Yenye maudhui

Na ili kukifunza vizuri kipengele hiki, itambidi mwalimu ajipangie makusudio yake mwenyewe ya kufunza kila sehemu yake. Kwa mfano sehemu ya (a) yasema fasihi ni sanaa; kwa

hiyo kusudi la kukifunza kigezo hiki darasani ni: Kuwafahamisha wanafunzi maana ya sanaa. Wakijua sanaa ni nini, sasa wataweza kuhusisha dhana hiyo na vitu mbalimbali na itakuwa pia rahisi kuwaleta wanafunzi hao katika dhana ya fasihi kuwa sanaa ya maneno. Uvunjaji wa vipengele hivi kuingia katika mada ndogo ndogo mbalimbali utafanyika pia kwa vipengele vinginevyo, na katika hatua mbalimbali.

Mkabala

Ili kufaulu, ni vizuri zaidi kuanza na mambo yanayofahamika kwa wanafunzi (fasihi simulizi kiutendaji si kitu kigeni kwa wanafunzi wetu) na kuendelea kwa yale yasiyo fahamika. Nadharia yetu ya kukabili taaluma 'Ki spiringi' inatufaa hapa. Kila hatua moja inayoeleweka, itumiwe kupanua na kujengea hatua inayofuata.

Mifano na mambo yanayofahamika kwa vijana yatumiwe ili kuwatoa kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine. Kwa mfano: mifano ya hadithi, methali, vitendawili, nyimbo inaweza kutolewa kutoka kwa wanafunzi wenyewe ili ichambuliwe na kujadiliwa. Majina ya fani na tanzu mbalimbali yanaweza yakapendekezwa na wanafunzi wenyewe. Vile vile kazi na dhamana anuai za fasihi simulizi. Kutokana na uchambuzi wa haya mambo yanayofahamika mwalimu na wanafunzi wataweza kuvifahamu na kuvigundua vipengele mbalimbali vya nadharia ya somo hili. Nia ni kumfunza mwanafunzi somo hili kwa kumfanya awe mchunguzi na aweze kugundua mambo (kwa kuongozwa).

Kwa mfano tu, wakati wa kufunza "tanzu za fasihi simulizi" katika kidato cha kwanza, mwalimu anaweza kuleta mifano ya aina mbalimbali darasani ambayo wanafunzi wataisikiliza kwa makini na kushiriki katika kuitenda. Baadaye, kwa msaada wake mwalimu, wanafunzi wajadili kwa nia ya kuainisha tungo hizo kwa fani, sifa, wadhifa n.k. Majibu mengi, mwalimu atagundua, yatatokana na wanafunzi wenyewe kwa vile wanazifahamu fani hizi nje ya darasa. Kazi ya mwalimu ni kuwasaidia kupanga ujuzi huo kitaaluma na kuwaelekeza pale penye ugumu wa kitaaluma.

Mbinu

Mbinu nyingi zaweza kutumiwa kufundisha. Mbinu kuu yamtegemea mwalimu na mwanafunzi wake kushiriki katika utendaji huo wa ujifunzaji kuchungua na kugundua pamoja. Baadhi ya mbinu anazoweza kutumia mwalimu zimetajwa katika Kiongozi cha Mwalimu (1978); lakini si vibaya kurudia kutaja hapa mbinu hizo:

(a) Majadiliano ya mwalimu na wanafunzi kwa kutumia data za fasihi simulizi, na kufikia mahitimisho mbalimbali.

(b) Wanafunzi kujadili wao kwa wao kwa vikundi na kupata maarifa kutokana na mada zilizopangwa kwa kutumia data za fasihi simulizi.

(c) Mihadhara ya wageni kutoka nje wakiwa ni wazungumzaji maalumu:

 i) ama wanataaluma wa fasihi simulizi.

 ii) ama ni wasanii.

(d) Kuhudhuria shughuli za kitamaduni zinazozingatia na kutumia fasihi simulizi.

(f) Kupanga warsha za utunzi, uchunguzi au uhakiki wa fasihi simulizi za darasa, za shule moja au zaidi.

(g) Kuandaa tafrija ambazo zitaonyesha matumizi na ibara za fasihi simulizi: mashindano au maonyesho tu. Tafrija hizi zitawasaidia wanafunzi kufanya uchunguzi na pia kuwawezesha kuujua usanii. Tafrija hizi zaweza kuwa ni za shule moja au zaidi. Hata pia za kitaifa.

(h) Kumbukumbu Waalimu na wanafunzi wanaweza kujenga kumbukumbu yao wenyewe ya uchunguzi wa fasihi simulizi ambayo wanaweza kuitumia katika shughuli zao za marejeo.

(j) Ziara:- mbalimbali zitakazosaidia kupanua mawazo ya mwanafunzi katika mwanya huu zitumiwe.

Vifaa

Vifaa navyo ni vya aina nyingi lakini vinategemea hali halisi ya uwezo wa shule wa kiuchumi.

a. Vitabu ni njia muhimu; lakini vitabu hivi hasa ni vile vya nadharia, aidha vile vya mikusanyo ambavyo vinaweza kutoa mifano.

b. Vinasa sauti vyaweza kutumiwa darasani kutolea mifano ya kuchambuliwa ili kuthibitisha hoja.

c. Ripoti za uchunguzi wa watu mbalimbali na za wanafunzi katika majarida na katika maktaba ya shule zinaweza kutumiwa.

d. Picha na Sinema za kimasomo kwa mfano kutoka Taasisi ya Vielelezo: "Somo Kasema" "Maisha" "Karibu" zitumiwe hasa kwa jinsi zinavyodhihirisha matumizi ya fasihi simulizi.

e. Wasanii mahiri wanaweza kualikwa waje darasani kuwatongolea au kuwatambia wanafunzi fasihi simulizi watakazotumia masomoni.

f. Mwalimu na wanafunzi wenyewe watoe mifano kwa vitendo.

Kwa jumla vifaa na mbinu zinazoweza kutumiwa katika somo hili ni vingi na vinategemea mazingira ya shule na darasa lenyewe.

Mwalimu, katika mazingira ya shule, anayo fursa ya kuibua mbinu na mizungu mbalimbali ili kuwezesha somo lifaulu. Vifaa navyo ni vingi na vya aina mbalimbali. Huu ni udokezi mfupi tu wa jinsi somo hili linavyoweza kukabiliwa. Udokezi wenyewe hauingii kwa undani sana.

TANBIHI

1. Vitabu ambavyo hadi sasa vinaongea juu ya nadharia ya fasihi simulizi kwa Kiswahili, kwa mfano tu ni:


Kirumbi, P.(1977) Misingi ya Fasihi Simulizi, Shungwaya Publishing House, Nairobi.

Muhando, P. na Balisidya, N.(1977) Fasihi na Sanaa za Maonyesho, T.P.H. DSM

Balisidya, M. Kitangulizi cha Fasihi Simulizi,(1975) Taasisi ya Elimu DSM (1981) University Press, DSM.

Balisidya, M.(1977) "Mabadiliko Katika Fasihi Simulizi ya Wagogo" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

2. Makala ya Fasihi Simulizi yametolewa katika majarida mbalimbali. Makala kwa lugha ya Kiswahili yamo katika KISWAHILI, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. MULIKA, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu, DSM. KIOO CHA LUGHA na ZINDUKO, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu, DSM. LUGHA YETU, Baraza la Kiswahili la Taifa, DSM. Pia yapo makala machache kutokana na Semina za Kimataifa za Waandishi wa Kiswahili, zilizofanywa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, kwa msaada wa UNESCO, 1978 na 1979.

3. Jambo hili linasisitizwa katika Muhtasari na Mwongozo wa Somo. Tazama katika Kiongozi cha Mwalimu cha Fasihi Simulizi 1-4, Taasisi ya Elimu, DSM.

4. Guthrie, na Greenberg, J. ni wana isimu wanaojaribu kuainisha lugha za Kiafrika.

5. Chiraghdin, S. "KISWAHILI NA WENYEWE", Kiswahili 44/1, March 1974 Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

6. Mikusanyo ya Fasihi simulizi kwa lugha ya Kiswahili na kwa lugha nyinginezo ipo mingi. Katika Afrika Mashariki kazi hii imefanywa kuanzia enzi za 1850. Mikusanyo mingi imechapishwa; lakini mingine mingi haijachapishwa. Mfano tu ya baadhi ya Wakusanyaji ni:

E. Steere, E. Tailor, C. Velten, A. Werner, W. Whitley,
L. Harries, J. Knappert, E. Dammann, C.G. Buttner,
E. Kezilahabi, D. Kamera, T. Sengo, S. Msuya, S. Farsy,
E. Meena, C. Omari, Baalawy, M. Khamis; na wengineo wengi.